# Shareholders **Calendar**

## Ilani ya Mkutano Mkuu wa Kila Mwaka

TAARIFA IMETOLEWA HAPA kwa Wenyehisa kwamba, kwa mujibu wa kanuni za vipengele vya sehemu ya 280 ya Sheria za Kampuni, 2015 na Hati ya Ushirika ya Kampuni, Kifungu cha 67, Mkutano Mkuu wa Sabini na tatu wa Kila Mwaka wa Kampuni ya Kenya Electricity Generating PLC utafanywa kupitia mawasiliano ya kielektroniki siku ya Alhamisi, tarehe 4 Decemba 2025 saa 5.00 asubuhi. kwa madhumuni ya kuzingatia na, ikiwa sawa, kupitisha maamuzi yaliyobainishwa hapa chini:

**Shughuli ya Kawaida**

1. Kuwasilisha majina ya washirika na kutambua uwepo wa idadi ya kutosha ya wanachama kuendesha mkutano.
2. Kusoma Taarifa inayoitisha mkutano
3. Kuzingatia na ikiidhinishwa, kupitisha Taarifa za Kifedha za Kampuni zilizofanyiwa ukaguzi kwa mwaka uliokamilika tarehe 30 Juni 2025, pamoja na Ripoti za Mwenyekiti, Wakurugenzi Watendaji na Wakaguzi waliomo.
4. Kuidhinisha malipo ya mgao wa mwisho wa mapato ya hisa wa Kshs. 0.90 kwa kila hisa ya kawaida ya Kshs. 2.50, inayotolewa kodi inayoshikiliwa panapohitajika, katika mwaka wa kifedha uliokamilika tarehe 30 Juni 2025.
5. Kujadili na kuidhinisha Ripoti ya Mshahara wa Wakurugenzi Watendaji na kuidhinisha malipo ya ada za Wakurugenzi Watendaji kwa mwaka uliokamilika tarehe 30 Juni 2025.
6. Wakaguzi: Kubaini kuwa ukaguzi wa vitabu vya akaunti za Kampuni utaendelea kufanywa na Mkaguzi Mkuu au na shirika la ukaguzi atakaloliteua kwa mujibu wa Sehemu ya 23 ya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya 2015.
7. Kuidhinisha Wakurugenzi Watendaji kusuluhisha malipo kwa Wakaguzi
8. Kuchagua Wakurugenzi
    i. Mheshimiwa Stephen Mutai ambaye anastaafu kwa awamu kulingana na Kifungu cha 126 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni,
    ii. Bi. Josphine Koisaba ambaye anastaafu kwa awamu kulingana na Kifungu cha 126 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni na
    iii. Bw. William Rahedi ambaye anastaafu kwa awamu kulingana na Kifungu cha 126 cha Hati ya Ushirika ya Kampuni na kwa kuwa anastahiki, anajitokeza kuchaguliwa tena kama Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni.
9. Kwa mujibu wa kanuni za Sehemu ya 769 za Sheria ya Kampuni ya 2015, wakurugenzi watendaji wafuatao, kwa kuwa wanachama wa Kamati ya Bodi ya Ukaguzi, Hatari na Utiifu ya Bodi wanachaguliwa kuendelea kuhudumu kama wanachama wa Kamati husika:
    i. CPA Bernard Ngugi
    ii. Bw. Stephen Mutai [Kutegemea iwapo atachaguliwa tena katika Bodi kulingana na kipengee cha 8(ii)]
    iii. Bi. Josphine Koisaba [Kutegemea iwapo atachaguliwa tena katika Bodi kulingana na kipengee cha 8(ii)]
    iv. Bw. Umuro Wario
    v. Bw. Kennedy Ondieki Mwakilishi wa Bw. John Mbadi (Waziri wa Fedha)
10. **AGENDA MAALUM**
    Uidhinishaji wa Sera za Kampuni
    Kutoa mamlaka kwa Bodi kuandaa, kuidhinisha na kupitia mara kwa mara HATI za sera kama jukumu endelevu linalotambuliwa chini ya Kanuni ya 8.21 ya Jedwali la Kumi na Tatu la Kanuni za Masoko ya Mitaji (Utoaji wa Hadharani, Uorodheshaji na Ufichuzi wa Taarifa), 2023 kwa:
    a. Sera ya Malipo
    b. Sera ya Ushirikiano na Mawasiliano na Washikadau
    c. Sera ya Mawasiliano Madhubuti na Washikadau
    d. Sera ya Utatuzi wa Migogoro
    e. Sera ya Kuhifadhi na Kuvutia Wajumbe wa Bodi ya Kampuni
11. Kuzingatia shughuli nyingine yoyote ambayo taarifa yake imetolewa

**Kwa Agizo la Bodi**

**FCS. Austin Ouko**
*Katibu wa Kampuni*

Novemba 13 2025